JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

BARAZA LA FAMASI

TAARIFA MUHIMU

DODOMA: 22 Novemba, 2026

Tunapenda kuwataarifu kuwa utoaji wa Namba za Malipo (*Control Number*) kwa kundi la kwanza umekamilika. Utoaji wa Namba za Malipo kwa Wahitimu katika **kundi la pili** (Wahitimu ambao walishauriwa na wanaendelea kufanya maboresho ya taarifa zao katika mfumo kupitia akaunti zao), utaanza **tarehe 24 Novemba, 2026** saa 2:00 asubuhi na namba hizo zitakwisha muda wake (*expired*) ifikapo tarehe **25 Novemba, 2026** Saa 5:59 usiku.

Kwa wahitimu ambao watakuwa hawajapata Namba za Malipo hadi kufikia tarehe 25 Novemba, 2026 saa 6.00 usiku, wanashauriwa kufika Ofisi za Baraza zilizo karibu kwa maelekezo zaidi.

Imetolewa na;
Msajili,
Baraza la Famasi,
DODOMA.